ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR

TAARIFA KWA UMMA

MAKUSANYO YA KODI YA NUSU MWAKA WA FEDHA 2023/2024 (JULAI - DISEMBA, 2023)

Zanzibar, 02 Januari, 2024.

1. MAKUSANYO YA JULAI - DISEMBA,2023

Mamlaka ya Mapato Zanzibar(ZRA) inautaarifu umma kwamba katika kipindi cha nusu mwaka wa Fedha, 2023/2024, cha Julai-Disemba,2023, **IMEFANIKIWA** kukusanya Jumla ya **Tshs. 351.768 Bilioni**, kati ya lengo la Kukusanya **Tshs. 335.382 Bilioni**, ambao ni **UFANISI** wa **asilimia 104.89** ya lengo la Makusanyo ya Kodi tarajiwa.

Aidha, katika nusu mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Makusanyo halisi ya kodi **YAMEONGEZEKA kwa asilimia 22.96**, na kwa kiasi cha **Tshs. 65.675 Bilioni**, ukilinganisha na mapato halisi ya nusu mwaka wa Fedha uliopita wa 2022/2023, ambayo yalikuwa ni **Tshs. 286.093 Bilioni**. Kipekee, kwa mara ya kwanza, ZRA, **IMEFANIKIWA** kuvuka lengo kwa kila mwezi ndani ya miezi yote sita ya nusu mwaka wa Fedha 2023/2024 (Julai - Disemba), na kufikia **UFANISI** wa **asilimia 104.89** (Jedwali Nam. 1 linatoa ufafanuzi zaidi)

Jedwali Na. 1: Makusanyo ya Mapato ya nusu Mwaka wa 2023/2024 (Julai- Disemba, 2023)

	2022/2023	2023/2024				
Mwezi	**Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)**	**Makisio (Tshs.In Billioni)**	**Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)**	**Ufanisi**	**Ukuaji**	**Ongezeko (Tshs.Billion)**
Julai	37.674	42.437	42.897	101.08%	13.86%	5.223
Agosti	46.248	55.616	57.238	102.92%	23.76%	10.990
Septemba	47.87	59.002	61.694	104.56%	28.88%	13.824
Octoba	48.682	58.120	61.201	105.30%	25.72%	12.519
Novemba	55.931	60.888	65.222	107.12%	16.61%	9.289
Disemba	49.685	59.318	63.514	107.07%	27.83%	13.828
Jumla	**286.093**	**335.382**	**351.768**	**104.89%**	**22.96%**	**65.675**

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Zanzibar

2. SABABU ZA KUFANYA VIZURI:

Ufikiaji wa lengo la Makusanyo ya Kodi wa zaidi ya **asilimia 104.89**, na ongezeko la kodi kwa **asilimia 22.79**, pamoja na mambo mengine umesababishwa na :

i. **KUIMARIKA** kwa shughuli za kiuchumi na uwekezaji wa miundombinu Zanzibar unaotokana na utekelezaji wa sera nzuri za kiuchumi za Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

ii. **KUONGEZEKA** kwa Uwajibikaji wa Ulipaji Kodi wa Hiari kwa walipakodi. ZRA, **TUNAWAPONGEZA** sana Walipakodi wote kwa Kutimiza Wajibu wao wa Kiraia wa Kulipa Kodi kwa Hiari;

iii. **KUONGEZEKA** kwa **UFANISI** wa watumishi wa ZRA kutokana na utekelezaji wa Muundo mpya wa ZRA, Uboreshaji wa huduma za kodi katika ofisi za Mikoa ya kikodi ya Unguja na Pemba, pamoja na matumizi ya mifumo ya ukusanyaji kodi ya VFMS na ZIDRAS; na

vi. **KUIMARIKA** kwa ushirikiano na Taasisi nyingine zinazofanya kazi na ZRA ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kamisheni ya Utalii na Ofisi za Uhamiaji.

3. ONGEZEKO LA MAKUSANYO YA KODI KATIKA MIAKA MITATU YA UONGOZI WA MHE. RAIS, DKT. HUSSEIN ALI MWINYI :

Wakati tunasherekea Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar na miaka mitatu(3) ya uongozi wa **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ufanisi** wa makusanyo ya kodi ya ZRA umeongezeka sana. Makusanyo ya **nusu mwaka (miezi sita)** katika mwaka wa tatu wa uongozi wa Mhe. Rais wa Zanzibar, ambayo ni **Tshs. 351.768 Bilioni**, ni makubwa kwa kiasi cha **Tshs. 47.425 Bilioni**, ukilinganisha na makusanyo ya mwaka mzima wa kwanza wa uongozi wake, kwa kipindi cha **Julai, 2020- Juni, 2021 (Miezi kumi na mbili)** yaliyokuwa ni **Tshs. 304.342 Bilioni**. Hii ni uthibitisho wa usimamizi mzuri wa sera za Uchumi wa Zanzibar, na ongezeko la ulipaji kodi wa Hiari Zanzibar kutokana na usimamizi wa Matumizi ya Kodi ambapo faida za kodi zinazoonekana waziwazi.

4. MIKAKATI YA NUSU YA PILI, JANUARI-JUNI, 2024:

Katika kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi katika nusu mwaka ya pili ya Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 (Januari- Juni, 2024), ZRA, itaendelea kufanya yafuatayo:

i. **KUSIMAMIA** miongozo ya **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya **kuimarisha mahusiano mazuri na walipakodi**, kuimarisha matumizi ya Mifumo katika usimamizi wa kodi ikiwemo matumizi ya **RISITI ZA KIELEKTRONIKI (VFD)**, matumizi ya **ZIDRAS**, na kukamilisha uunganishaji (Integration) wa baadhi ya Mifumo ya wafanyabiashara na Mfumo wa VFMS.

ii. **KUIMARISHA HUDUMA** za Kodi (Elimu ya Kodi, Usajili wa kodi, Uwasilishaji wa Ritani , Malipo ya Kodi na Ukaguzi wa Kodi) katika ofisi za kodi za Mikoa na vituo vya huduma za kodi (Tax Service Centres), pamoja na kuimarisha ZRA call centre, ili kurahisisha ulipaji kodi wa hiari Zanzibar;

iii. **KUENDELEZA WELEDI WA WATUMISHI** wa ZRA kwa kuwapatia mafunzo stahiki, usimamizi makini, huduma nzuri kwa walipakodi (Customer care) pamoja na kuchukua Hatua zinazofaa.

vi. **KUSIMAMIA** uwajibikaji wa hiari kwa walipakodi wakubwa, wakati na wadogo kwa kuwasaidia kurahisisha biashara zao na usimamizi wa usawa katika ulipaji kodi.

v. **TUNAWATAKIA WALIPAKODI NA WANANCHI WOTE, HERI YA MWAKA MPYA WA 2024,PAMOJA NA HERI YA MIAKA 60 YA MAPINDUZI MATUKUFU YA ZANZIBAR.**

"Tulipe Kodi Kwa Maendeleo ya Zanzibar"

Yusuph Juma Mwenda
KAMISHNA MKUU